





# Kununua nguo

 Espen Stranger-Johannessen

 Sara Sahar Haidari

 Jacob Haule

 3

 Kiswahili SW



Shati la Ali limechakaa. Anahitaji jingine jipya.



Anaenda madukani kununua nguo mpya.



Akiwa madukani, haoni duka la nguo.



Anaenda dukani kuulizia uelekeo. “Wapi ninaweza kununua nguo?” Anauliza.



Muuzaji anaonyesha upande wa pili wa maduka.  
Duka la nguo lipo upande wa pili.



Ali anaingia na kuangalia mashati. Mashati ni makubwa mno kwake na ni ghali sana.



Badala yake, ananunua suruali mpya kwa sababu zinauzwa. Anaamua kwamba atanunua shati mwezi ujao atakapopata mshahara wake.





# LIDA Stories

[lidastories.net](http://lidastories.net)

## Kununua nguo

 Espen Stranger-Johannessen

 Sara Sahar Haidari

 Jacob Haule

